**MAMLAKA YA USIMAMIZI WA SHUGHULI ZA BIMA (TIRA).**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KATIKA UZINDUZI WA WARAKA WA MAMLAKA NAMBA 55/2017**

**Ndugu waandishi wa Habari:**

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA), leo tarehe 11Desemba 2017 inazindua waraka ujulikanao kama "**Waraka Na.055/2017 (Masharti ya Kufanya Biashara na Makampuni Ya Bima Mtawanyo na Madalali wa Bima Mtawanyo Kutoka Nje ya Nchi**".

Waraka huu utaanza kutumika rasmi kuanzia **Jumatatu** ya tarehe **1 mwezi Januari 2018.** Waraka huu ni moja ya jitihada za Mamlaka za kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kutokana na kupeleka biashara za bima nje ya nchi kupitia utaratibu ujulikanao kama bima mtawanyo au ***"reinsurance"*** kwa lugha ya kiingereza.

**Ndugu waandishi wa Habari,**

Naomba itambulike kuwa utaratibu wa kupeleka biashara za bima nje ya nchi ni suala la kawaida katika masoko ya bima duniani, hivyo, utaratibu huu unapofanyika vizuri huleta faida anuai kwa soko la ndani kama ifuatavyo:

i. **Kushirikisha makampuni ya bima ya nje katika kulipa hasara zitokanazo na majanga ya ndani ya nchi:** ambapo tozo na madai yanayotokana na kupeleka biashara nje hutawanywa kwa uwiano unaokubalika kati ya makampuni ya bima yaliyoko nchini na makampuni ya bima mtawanyo ya nje ya nchi;
ii. **Kuimarisha mapato na mitaji ya makampuni ya bima ya ndani:** hii ni kutokana na tozo na ada (reinsurance commission) yanayolipa makampuni ya bima mtawanyo ya nje ya nchi kwa makampuni ya bima nchini kutokana na biashara wanayopokea kutoka makampuni ya ndani;
iii. **Usimamizi mzuri wa madai:** uwiano wa kulipa madai kwa makampuni ya ndani huimarika kutokana na makampuni ya nje

kushiriki katika ulipaji wa sehemu ya hasara ambazo makampuni ya ndani hupata;

iv. **Kuimarisha uwezo wa kitaalam wa watendaji katika sekta ya bima nchini:** Watendaji wa sekta ya bima nchini watapata ujuzi kutoka kwa wataalam wa nje wenye uzoefu katika mambo ya bima na bima mtawanyo;

v. **Kulinda mitaji ya makampuni ya bima nchini:** Mitaji ya makampuni ya bima nchini hulindwa dhidi ya athari za madai makubwa ya bima kwa kuwa sehemu ya madai hayo hulipwa na makampuni ya bima mtawanyo ya nje ya nchi.

**Ndugu Waandishi wa Habari:**

Utaratibu wa kupeleka biashara za bima nje ya nchi usipotumika vizuri kwa maana ya viwango vya upelekaji wa biashara za bima nje ya nchi kuzidishwa na kutotumia kikamilifu uwezo wa soko la ndani; hasara mbalimbali hulipata soko la bima nchini zikiwemo zifuatazo:

a) Kuwanyima wafanyabiashara wa ndani fursa ya kukuza mitaji yao na kufikia idadi kubwa ya wateja kutokana na kutoshirikishwa katika mjanga yanayokingwa nchini.

b) Kurudisha nyuma uwezo wa kitaalamu wa soko la ndani katika kushughulikia majanga makubwa na magumu ambayo huendelea kushughulikiwa na makampuni ya bima mtawanyo ya nje ya nchi.

c) Kupunguza mchango wa sekta ya bima katika uchumi wa nchi kutokana na sehemu ya mapato ya makampuni ya bima kupelekwa nje ya nchi. Mapato hayo yangewekezwa katika amana za mabenki na aina nyingine ya uwekezaji na hivyo kuchangia katika ukuzaji wa mitaji nchini.

**Ndugu Waandishi wa Habari:**

Mamlaka imebaini matumizi hasi ya utaratibu wa kupeleka nje biashara za bima mtawanyo kwa baadhi ya makampuni ya bima nchini katika maeneo yafuatato:

(i) Matumizi yaliyopindukia ya taratibu za kimataifa za bima mtawanyo za makubaliano ya papo-kwa-papo *("International Facultative Reinsurance Arrangements")* hata kwenye mazingira ambayo biashara husika zingeweza kufanyika kwa njia ya bima mtawanyo ya mikataba *("Treaty Reinsurance Arrangements");*

(ii) Upelekwaji wa biashara ya bima kwa asilimia mia moja nje ya nchi ("fronting of risks") ambapo sehemu yake ingeweza kubakizwa nchini;

(iii) Ushiriki hafifu wa makampuni ya bima nchini katika kutoa bima za majanga makubwa na magumu (large and complex risks);

(iv) Baadhi ya makampuni ya bima nchini kupendelea kushirikisha makampuni tanzu yaliyo nje ya nchi katika kutoa kinga za bima nchini badala ya kushirikisha makampuni ya bima ya hapa nchini *("co-insurance arrangements with sister or parent companies based in other jurisdictions");*

(v) Baadhi ya makampuni ya bima nchini kufanya biashara za bima na makampuni ya bima mtawanyo yasiyo na viwango bora vya ithbati;

(vi) Kufanya biashara na makampuni ya bima mtawanyo na madalali wa bima mtawanyo nje ya nchi bila kuzingatia hali zao kisheria, kiutendaji na kifedha;

(vii) Kukosekana kwa uwazi kuhusu viwango na mahali zinapolipwa ada na kamisheni za bima panapotumika mlolongo wa madalali wa bima mtawanyo;

(viii) Baadhi ya makampuni ya bima kuomba kupeleka nje ya nchi biashara za bima ambazo muda wake umekwisha au unakaribia kwisha; na

(ix) Kukosekana kwa uwazi wa kutosha kuhusu mapato (ada na kamisheni) yatokanayo na biashara ya bima kupelekwa nje ya nchi ("*reinsurance commission/ fronting fee*").

**Ndugu waandishi wa Habari.**

Kwa kuzingatia mapungufu hayo hapo juu, Mamlaka imetoa waraka No**. 55/2017** ili kudhibiti mwenendo hasi na kuimarisha ufanisi katika upelekaji wa biashara za bima mtawanyo nje ya soko la bima la Tanzania.

Ni matarajio ya Mamlaka na Makampuni ya bima hapa nchini kuwa utekelezaji wa waraka huu utaimarisha ufanisi wa soko la bima katika tasnia nzima ya bima mtawanyo na kuwezesha Serikali kupata mapato stahiki kutoka sekta ya bima. Faida hizo ni pamoja za zifuatazo:

i. **Kuimarisha kiwango cha tozo za bima zinazobakizwa hapa nchini hivyo kuongeza kiwango cha mchango wa sekta ya bima katika rasilimali fedha na uchumi wa ndani:** Tozo zitakazokuwa zimebakizwa nchini zitawekezwa katika taasisi na mifumo ya fedha ili kukuza mitaji ya ndani.

ii. **Kuyapa makampuni yote ya bima nchini fursa ya kuimarisha mapato yao** kutokana na kuongezeka fursa za kushirikishwa katika utoaji wa kinga kwa bima ambazo zingeweza kupelekwa nje ya nchi.

iii. **Kuimarisha uwezo wa kitaalam na kimtaji wa soko la bima la ndani** katika kushugulika na majanga makubwa na magumu ambayo kwa sasa hupelekwa katika masoko ya nje.

iv. **Kuongeza ubora na imani ya wananchi kwa huduma za bima zinazotolewa nchini;** kutokana na waraka kuyataka makampuni ya bima mtawanyo na madalali wa bima mtawanyo wa nje ya nchi kupewa ithibati ndani ya nchini. Makampuni ya bima hapa nchini pia yatatakiwa kuhakikiwa uwezo wa kifedha na uhimili wa kulipa ahadi (***credit-rated)*** angalau mara moja kila baada ya miaka mitatu.

v. **Kuongeza umakini wa makampuni ya bima nchini katika upangaji wa viwango vya tozo za bima** kwa kuwa utaratibu huu utaambatana na kuimarishwa kwa vigezo vya upangaji wa mitaji vinavyozingatia vihatarishi (risk based capital requirements) sambamba na kuwekwa wazi kwa viwango vya kamisheni na ada zinazolipwa kwa makampuni ya bima nchini kutokana na bima mtawanyo.

**Ndugu Waandishi wa Habari:**

Waraka huu umetolewa baada ya Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima nchini (TIRA) kuhusisha wadau husika wa sekta ya bima ndani na nje nchi.

Mamlaka inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kisheria, ikiwa ni taasisi yenye jukumu la kuishauri serikali kuhusu masuala ya bima. Mamlaka inawajibika pia kusimamia na kuendeleza soko la bima nchini ili kuwalinda walaji wa bima na kuchangia katika uchumi wa nchi.

Mamlaka imejidhatiti kutekeleza majukumu yake chini ya Serikali ya Awamu ya Tano ya **Mh. Dr. John Pombe Magufuli,** katika dhamira ya kujenga uchumi wa viwanda kwa kutoa huduma za bima kwa watanzania na makampuni ya kitanzania, kutengeneza fursa za ajira kwa watanzania na kuongeza mchango wa sekta ya bima katika pato la taifa.

Dr. Baghayo A. Saqware
**Kamishna wa Bima.**